Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 – 9289]



**Issue no:** 01 | **Vol no:** 06 | **August** 2025: 35-43

# Uchunguzi wa Dhamira Zinazojengwa na Vipengele vya Sanaa katika Visasuli vya Wahaya

**Farida Hassan Kyabalishanga**[1]
**Joviet M. Bulaya**[2]
**Leonard Bakize**[3]

**(1.2.3)** Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
Main author's email: faridakyabalishanga11@gmail.com

**Article History**
Received: **2025.06.17**
Accepted: **2025.07.16**
Published: **2025.08.18**

**Cite this article in APA**
Kyabalishanga, F. H., Bulaya, J. M., & Bakize, L. (2025). Uchunguzi wa dhamira zinazojengwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vya Wahaya. *Editon consortium journal of kiswahili*, *6*(1), 35-43. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v6i1.616

**Ikisiri**
Sanaa ni sehemu muhimu ya maisha ya kila siku katika kabila la Wahaya. Umuhimu wa sanaa katika kabila la Wahaya unatokana na utajiri mkubwa walionao katika fasihi simulizi hususani visasuli. Licha ya utajiri huo bado inaonesha kuwa maandiko mengi ya kisanaa na kihistoria hayakuandikwa hali iliyosababisha kutokuwapo kwa tafiti za kutosha kuhusu visasuli vya kabila la Wahaya. Makala hii imechunguza dhamira zinazojengwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vya Wahaya. Sababu ya uchunguzi huu ni kwamba vipengele vya sanaa vimekuwa vikichunguzwa kwa ujumla sana katika kazi za fasihi bila ubayana unaoonesha namna vipengele hivyo vinavyojenga dhamira katika visasuli, hususani visasuli vya Wahaya. Data za makala hii zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya mahojiano. Mjadala wa kimsingi katika Makala hii umekitwa na kuongozwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliyoasisiwa na Wolfgang Iser (1978), Stanley Fish (1980) James Tompkins (1980), Haus Robert Jauss (1982) na Robert Holub (1984), katika ukusanyaji na uchambuzi wa data za makala hii. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa vipengele vya sanaa katika visasuli vya Wahaya vinatumika kujenga dhamira. Dhamira hizo ni pamoja na matumizi ya vifaa jadi wakati wa kula, kuonesha thamani ya kitu unachokimiliki, kuharibika kwa maadili, kuendeleza utamaduni, uzazi, mahari, na huruma kwa wahitaji.

**Key words**: Dhamira, sanaa, visasuli, wahaya.

Editon OPEN ACCESS

CC BY NC SA
This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Visasuli kama aina ya hadithi fupi za kubuni hujengwa kwa ustadi kupitia vipengele vya sanaa kama vile taswira, tamathari za semi, migogoro, ucheshi na matumizi ya lugha fasaha kwa lengo la kukamilisha mawasiliano yaliyokusudiwa. Aidha, visasuli hutoa nafasi kwa jamii kujitathmini kupitia wahusika wa kubuni kwa lengo la kuonesha uhalisia wa maisha ya jamii. Naye Okpewho (1992) anaeleza kuwa vipengele vya sanaa katika visasuli ni njia za ubunifu zinazosaidia kuwasilisha dhamira kuu na kuifanya kazi ya fasihi kuwa na mvuto wa kipekee. Miongoni mwa jamii zinazotunza kwa dhati urithi wa visasuli ni jamii ya Wahaya ambao wamekuwa na mchango mkubwa katika kuhifadhi maarifa na maadili kupitia visasuli.

Katika muktadha wa jamii ya Wahaya visasuli hujengwa kwa ustadi mkubwa wa kisanaa unaobeba dhamira mbalimbali zinazolenga kuonesha mtazamo wa jamii kuhusu maisha, maadili na mfumo wa kijamii. Katika jamii ya Wahaya dhamira hujitokeza kwa namna mbalimbali kupitia matumizi ya vipengele vya kisanaa hususani visasuli. Hivyo, vipengele vya kisanaa si mapambo tu ya kisanaa bali ni vihusishi muhimu vya maana vinavyobeba dhamira mbalimbali. Licha ya utajiri mkubwa wa fasihi simulizi katika jamii ya Wahaya hakuna maarifa ya kutosha yanayoonesha vipengele vya sanaa katika visasuli vya jamii ya Wahaya na dhamira zinazoibuliwa kupitia visasuli. Hali hii inasababisha kukosekana kwa uelewa na maarifa ya namna sanaa ya visasuli vinavyoakisi, eleza na kukosoa mienendo ya jamii hiyo.

Data za makala hii, zimedondolewa kutoka visasuli vya kabila la Wahaya. Uteuzi wa jamii ya Wahaya ulitokana na sababu kwamba, wana sanaa na miiko katika masimulizi ya visasuli vyao na baadhi wanatumia miiko katika ujenzi wa maadili katika jamii hiyo. Mjadala wa makala hii umewasilishwa katika vipengele vifuatavyo: methodolojia ya utafiti, Nadharia ya uchambuzi wa data, uchambuzi na uwasilishaji wa data pamoja na hitimisho.

## MAPITIO YA MAANDISHI

Tafiti mbalimbali zimefanyika kuhusu visasuli. Mathalani, Mulokozi (2017) anaeleza kuwa visasuli ni vipera vilivyomo katika utanzu wa ngano. Mulozi anafafanua zaidi kuwa visasuli husimulia kuhusu chimbuko au asili ya jambo kama vile kiumbe fulani, mmea au mila fulani. Aidha, mtazamo mwingine unaotofautiana na Mulokozi unadai kuwa visasuli ni masimulizi ya kubuni yaliyotungwa kuelezea kisa au chanzo cha jambo linalosimuliwa kwa dhamira ya kufikisha ujumbe kwa wasimuliwaji (Rwabushaija, 2002). Licha ya kuwapo kwa vipengele vya sanaa katika visasuli bado uchunguzi wa namna vipengele hivyo vinavyojenga dhamira hauko bayana. Kutokana na umuhimu wa visasuli katika fasihi simulizi utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira zinazoibuliwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vya kabila la Wahaya. Lengo likiwa ni kujenga uelewa na maarifa ya namna dhamira zinazojengwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vinavyoakisi, eleza na kukosoa mienendo ya jamii hiyo.

### Nadharia ya Utafiti

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ni mabadiliko ya jumla ya umakinikaji kutoka kwa mwandishi na kazi yake kwenda kwa matini na msomaji (Fish, 1980). Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na wahakiki wa Kijerumani mwishoni mwa miaka ya 1960. Miongoni mwa waasisi na watetezi wakuu wa nadharia hii ni Wolfgang Iser (1974, 1978), Stanley Fish (1980), James Tompkins (1980), Haus Robert Jauss (1982) na Robert Holub (1984). Waasisi hawa wanafafanua kwamba, maana katika matini ya fasihi haiwezi kuonekana ikiwa itatenganishwa na uzoefu wa msomaji wa matini husika.

Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji inaakisi mabadiliko ya mbinu katika historia ya fasihi na ilizingatiwa kama jibu kwa jamii, wanazuoni na maendeleo ya fasihi huko Ujerumani Magharibi mwishoni mwa miaka ya 1960 na kuchukuliwa kama njia ya kimapinduzi kwa wahakiki wa kisiasa (Holub, 1984). Aidha, nadharia hii ina misingi mbalimbali kulingana na Holub (1984) ambayo ni: mwitiko wa msomaji huathiliwa na maarifa na tajiriba aliyonayo msomaji, maana ya msomaji hutokana na saikolojia yake na mwitiko wa msomaji huathiliwa na masuala ya kijamii na kiutamaduni yanayomzunguka msomaji. Makala hii haikuweza kutumia misingi yote isipokuwa imeongozwa na msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi kutoka msomaji mmoja na mwingine alioutoa Holub (1984). Mhimili huu ulimpa mtafiti maarifa ya kuweza kuchambua dhamira zinazojengwa na vipengele vya kisanaa kutoka visasuli vya Kihaya.

## MBINU ZA UTAFITI

Data za Makala hii zilikusanywa kutoka visasuli vya kabila la Wahaya. Wango la utafiti huu lilikuwa la uwandani kwa wenyeji wa Mkoa wa Kagera, Wilaya ya

Misenyi, tarafa ya Kiziba, kata ya Kanyigo. Waliangaliwa wenyeji wenye kujua masimulizi ya visasuli vilivyohifadhiwa vichwani mwao sio vilivyohifadhiwa kwenye maandishi, walisimulia wenyewe. Utafiti huu ulitumia wango hili kwa sababu masimulizi ya visasuli yaliyochunguzwa yanatumia sanaa iliyosheheni katika masimulizi hayo ili kufikisha ujumbe kwa wasikilizaji. Data hizo zilipatikana uwandani kwa njia ya mahojiano. Baada ya mahojiano hayo vipengele vya kisanaa vilidondolewa kutoka visasuli vya kabila la Wahaya.

Data kutoka visasuli vya Kihaya zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya kusimba maudhui ambayo huchanganua data kwa kutathimini hali ya matukio katika jamii. Kupitia mbinu hii, hatua zifuatazo zilifuata: mosi, kuzizoea data baada ya kusikiliza mahojiano na kuzidondoa kutoka visasuli vya Wahaya. Pili, mtafiti alitengeneza misimbo mbalimbali kwa kuzingatia madhumuni ya makala hii; na tatu misimbo iliyoendana na makala hii iliunganishwa. Data zilizokusanywa kutoka visasuli vya Kihaya zilichanganuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo ili ziweze kueleweka zaidi.

## MATOKEO NA MAJADILIANO

Sehemu hii inahusu matokeo na mahojiano ya data zilizopatikana kutoka visasuli vya Kihaya. Katika masimulizi ya visasuli hivyo vimeangaziwa vipengele vya sanaa vinavyoumba dhamira kutoka visasuli vya Wahaya. Katika sehemu zinazofuata, makala hii imechunguza na kubainisha vipengele vya kisanaa vinavyoibua dhamira katika visasuli vya Wahaya. Vipengele hivyo ni kama vile: tashibiha, tashihisi, takriri, sitiari, tafsida, methali, na kejeli. Makala hii imeonesha jinsi vipengele vya kisanaa katika visasuli vya Kihaya vinavyojenga dhamira. Kutokana na data za utafiti huu, vipengele hivi vya kisanaa ndivyo vinatumika kujenga dhamira katika visasuli vya Kihaya. Sehemu inayofuata, imejadili vipengele vya kisanaa kutoka visasuli vya Wahaya kama ifuatavyo:

### Tashibiha

Tashibiha ni tamathali ya semi inayolinganisha vitu viwili kwa kutumia kihusishi *kama* au *mithili ya* (Kitundu & Malangwa, 2019). Utafiti huu, umebaini kuwa tashibiha ni miongoni mwa kipengele cha kisanaa kinachopatikana katika visasuli vya kabila la Wahaya. Lengo la matumizi ya tashibiha katika jamii ya Wahaya ni kuibua dhamira kwa kufananisha vitu viwili au zaidi. Aidha, tashibiha ni moja katika vipengele maarufu katika tamathali za semi kinachotumika sana katika fasihi simulizi na pia katika fasihi andishi (Wamitila, 2003). Katika jamii ya Wahaya tashibiha imebainishwa kupitia msimuliaji wa visasuli aliyesema:

> **Kihaya**: *"Olwo Enyange yabaile nemala kugamba etakamizile kachwanta, Ekikona kilaisa omunwa nkendosho kiti aba abana bange wabona inye tindakuzala abana baikwera? Manya nanye nina ekikwela omungoto/ omubikya Nke ndosho."*
>
> **Kiswahili:** Enyange alipokuwa anamaliza kuongea hajameza mate, Ekikona alinyoosha mdomo kama jana la mgomba lililokunjwa kama kijiko, akasema kuwa hawa watoto ni wangu. Umeona mimi siwezi kuzaa watoto weupe? Si na mimi nina alama nyeupe shingoni. Enyange anadai kuwa watoto ni wake lakini Ekikona akanyoosha mdomo kiasi cha kuufananisha mdomo na jani la mgomba lililokunjwa mfano wa kijiko.

Dondoo hili linaonesha kuwa kuna miiko ya mazungumzo katika jamii ya Wahaya. Aidha, neno *nkendosho* ni tashibiha iliyotumika kufafanisha mdomo wa Ekikona na jani la mgomba lililokunjwa kama kijiko. Hii ina maana kitendo cha Ekikona kutoa mdomo kama jani la mgomba baada ya kuambiwa watoto si wake si tabia nzuri katika jamii ya Wahaya. Ni mwiko kunyoosha mdomo kumjibu mtu kwa jeuri au kumkatisha kabla hajamaliza kuongea. Kadhalika, tashibiha kama kipengele cha kisanaa kimetumika kuonesha ufanano kati ya mdomo na jani la mgomba lililokunjwa. Hussain (2014) anafafanua zaidi kuwa vitu viwili halisi vinavyolinganishwa huonesha mshabaha fulani wa sifa, sura na tabia ya mtu. Kadhalika, msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi, umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa kipengele cha tashibiha kimetumiwa kisanaa na msimuliaji kurejelea ujadi unaoakisi maisha halisi ya heshima kwa Wahaya kupitia visasuli.

### Matumizi ya Takriri

Takriri ni usemi unaojidhihirisha katika kifungu cha maneno kwenye mfululizo na mfuatano wa sentensi (Khatib, 1999). Kama mujibu wa Wamitila (2008) takriri ni mbinu ya kisanaa inayorejelea urudiaji au ukariri wa neno au sauti fulani. Katika makala hii imebainika kuwa

takriri katika visasuli vya Wahaya ni mbinu ya kurudiarudia jambo kwa kusudi maalumu la kumiliki. Mtunzi anaweza kurudiarudia maneno fulani, au silabi fulani kwa shabaha maalumu (Mulokozi, 1996). Katika utafiti huu, imebainika kuwa matumizi ya takriri kama mbinu ya kisanaa katika visasuli vya Wahaya yanalenga kutilia mkazo au msisitizo wa jambo linalosemwa na kurahisisha kuliweka akilini mwa msikilizaji anayesimuliwa. Dai hili limethibitishwa na msimuliaji aliposema:

> **Kihaya:** *Ekyawe kyawe nolwo kyakuba kili kitai.*
>
> **Kiswahili:** Chako ni chako hata kama kipo vipi.
>
> **Kihaya:** *Bailize hai abhana mbatemeteme.*
>
> **Kiswahili:** Wasogeze karibu watoto niwakatekate.

Data hapo juu inaonesha takriri ya "*Ekyawe kyawe*" imetumiwa kuweka msisitizo wa kuonesha thamani ya kitu chako sio kutamani kitu kisichokuwa chako. Vilevile, uchambuzi uliofanyika katika data hapo juu, umebaini kuwa takriri katika visasuli vya Wahaya inalenga kuamua utofauti unaojitokeza baina ya watu katika jamii. Kwa mfano, msimuliaji alipoonesha mfalme aliporudia neno "*temeteme*" lenye maana ya katakata alimaanisha wasogezwe karibu watoto awakatekate. Aidha msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi, umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa lengo la matumizi ya takriri si kuwakatakata watoto bali takriri ya "temeteme" ilitumiwa kwa lengo la kuonesha msisitizo ili kuweze kugundua mama halali wa watoto.

**Matumizi ya Sitiari**

Sitiari ni mbinu ya kisanaa ambayo hulinganisha vitu viwili visivyo na uhusiano wa moja kwa moja bila kutumia viunganishi vya mithili ya, mfano wa, sawa na, kama na kadhalika (Omari, 2006). Ulinganishi unahusisha mada pamoja na kibebeo kutokana na uhusiano wa kisemantiki (Fadaee, 2006). Utafiti huu umebaini kuwa katika visasuli vya Wahaya sitiari hulenga kuonesha tabia isiokubalika katika utamaduni wa jamii ya Wahaya. Hili limethibitishwa na msimuliaji aliposema:

> **Kihaya:** *Bagambila iba mukazi bati mkazi wawe njoka kandi njoka enjuju, koliwo nayekola namwenda.*
>
> **Kiswahili:** Walimwambia mume wa yule mwanamke kuwa Mkeo ni nyoka tena ni nyoka enjuju, ukiwepo anajifanya kupenda.

Dondoo hili linaonesha sitiari ya mke na nyoka ambayo haina uhusiano wa moja kwa moja kati ya mke na nyoka. Utafiti huu umebaini kuwa sitiari katika visasuli vya Wahaya inatumika kwa lengo la kuonesha unafiki. Suala la unafiki limefafanuliwa na John (2023) kuwa unafiki hudhihirika zaidi wakati mhusika anapoonesha kuwa ana upendo wakati hana upendo. Kwa hiyo, katika data hapo juu, tabia ya unafiki ya mwanamke inalinganishwa na nyoka anayeonekana hana madhara wakati ana madhara kwa binadamu.

**Matumiazi ya Tasifida**

Tasifida ni maneno ya miiko (Wambua, 2009). Aidha, tasifida ni chombo muhimu na maalumu cha mawasiliano katika jamii yoyote (Nguti, 2013). Uchambuzi wa data umebaini kuwa tasifida katika visasuli vya jamii ya Kihaya hutumiwa kama mbinu ya kisanaa ya kupunguza ukali wa maneno. Katika jamii ya Wahaya masimulizi yao huzingatia maneno ya tafsida kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno. Hili limebainishwa na mtoa taarifa kupitia tafsida ifuatayo:

> **Kihaya:** *Aho nilwo olushengo lwabandize, empu kazayomile zimuniga olwokuba zikamuganda amubili. Zimuniga abanza kutaba nokwikya abanza kwikya kubi, aho ayenda kugya kwejuna olwokuba abanilwe. Nokwo gwabaile guli muzilo kuzoka nayenda kwejuna omumaisho ga abantu, akabanza kulila nayeta bamujune omunaku zokumigwa nokwikya kubi chonka eilaka tilyashooile bakamuulila alai nashaba ajunwe. Balinya abasigazi tibamanyile kyakukola bwangu olwokuba amagezi gabo gakawelaho, chonka obutini bwabo nehali okwo yabaile eli a'Mukama babanza kuteleyombo.*
>
> **Kiswahili:** Maana yake ni kwamba, hapo ndipo balaa lilianza, ngozi zile zilikauka na kumkaba kwa kuwa ziliganda kwenye maungo. Akaanza kuteseka kwa kubanwa kiasi cha kumzuia kupumua vyema, wakati huo huo haja

> ya kwenda haja kubwa na ndogo zilimbana. Na kwa kuwa ulikuwa mwiko kuonekana na kujisaidia mbele za watu hali ile ilimzidia alianza kulia kwa sauti japo haikutoka vizuri lakini ilisikika akiomba asaidiwe. Wale wavulana hawakujua cha kufanya haraka kwa kuwa akili zao ziliishia hapo, lakini kwa uoga wao na hali ilivyokuwa kwa Mfalme walianza kupiga kelele.

Kutokana na data hii, tunaona kuwa matumizi ya tafsida katika visasuli vya Wahaya hulenga kuwajenga watoto katika maadili yanayoendana na utamaduni wao. Utafiti huu umebaini kuwa matumizi ya mbinu ya tafsida yamejitokeza wakati wa kuelezea masuala ya haja kubwa na ndogo. Maelezo ya Kandagor (2013) yanafafanua zaidi kuwa lengo la tafsida ni kuficha ukali wa maneno. Tofauti na utafiti ni kwamba katika visasuli vya Wahaya tafsida inatumiwa kwa lengo la kuendeleza miiko inayodumisha utamaduni wa Kihaya kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Matumizi ya Methali**

Wamitila (2008) anaeleza kuwa methali ni semi za kimapokeo zinazokumbukika na zenye muundo fulani unaotambulika na wanajamii na unaoelezea uzoefu unaokubalika na wanajamii kama ukweli fulani. Uchambuzi wa data za utafiti huu umebaini kuwa katika visasuli vya Kihaya methali ni mojawapo ya mbinu ya kisanaa inayotumiwa kujenga dhamira. Methali zilizobainishwa katika visasuli vya Wahaya zimenukuliwa kama ifuatavyo:

> **Kihaya:** *Obushasi bwomwana bumanywa nyina.*
>
> **Kiswahili:** uchungu wa mtoto aujuaye ni mama.

Dondoo hili linaonesha kuwa methali zinalelenga zaidi kuonesha tofauti kati ya mtu aliyezaa na asiyezaa katika jamii ya Wahaya. Hali hii inadhihirika kupitia suala la ujenzi wa maadili. Utafiti huu umebaini kuwa tofauti za ujenzi wa maadili katika jamii ya Wahaya hususani kwa wazazi waliojaliwa kuwa na watoto na wale ambao hawana watoto hupelekea kuibuka kwa methali. Maitaria (2013) anaeleza kuwa methali ni miongoni mwa semi fupifupi zilizobuniwa kutokana na mazingira halisi ya watu. Aidha, msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi, umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa, katika visasuli vya Wahaya methali ni kielelezo cha masuala muhimu katika utamaduni wa jamii.

**Matumizi ya Kejeli**

Kejeli ni usemi ambao kisemwacho sio kikusudiwacho na msemaji; kisemwacho kumbe ndicho kinabeuliwa (Ntarangwi, 2004). Katika fasihi, mbinu ya kejeli imetumiwa na inaendelea kutumiwa na waandishi ili kuiwezesha hadhira kufikiria kwa undani suala linaloongelewa ili kupata ujumbe uliokusudiwa kufikishwa kwao (Mrikaria, 2010). Utafiti huu umebaini kwamba, katika visasuli vya jamii ya Wahaya kejeli ni usemi unaotumia maneno ambayo huwa ni kinyume na maana lengwa. Kwa mfano, maneno ya kusifia au kupongeza kinyume chake ni dharau au kusuta. Hili limethibitika kupitia mtoa taarifa aliyesema:

> **Kihaya:** *Bashwela nka abajugile*.
>
> **Kiswahili:** Kuna wanaume wanawamiliki wake za watu kama wao ndiyo waliotoa mahari (wanalala nao).

Katika dondoo hili, utafiti huu umebaini kuwa kejeli kama mbinu ya kisanaa imetumiwa kuwakejeli wanaume wanaolala na wake za watu kama wao ndiyo waliotoa mahari. Aidha, katika makala hii imebainika kuwa kejeli inatumika zaidi katika visasuli vya Kihaya katika masuala yahusuyo mahusiano ya kingono na wake za watu. Pia, kejeli hutumiwa kama mbinu katika muktadha maalumu kwa lengo la kuelimisha, kukosoa pamoja na kuyaweka wazi mambo yaliyopo katika jamii kulingana na matukio na mabadiliko katika jamii (Mrikaria, 2010). Vilevile, maarifa na tajriba aliyonayo mtafiti kama ilivyoelezwa na Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji imemuongoza mtafiti kubaini kuwa katika jamii ya Wahaya kejeli hutumiwa kwa dhamira ya kuwakataza, kuwaonya wazazi wenye tabia ya kuwapenda watoto wao kupita kiasi na kuwaachia wafanye watakavyo.

**Matumizi ya Misemo**

Utafiti huu umebaini kuwa misemo ni miongoni mwa vipengele vya sanaa vinavyojitokeza katika visasuli vya Wahaya. Misemo ni fungu la maneno lenye maana maalumu, ujumbe kwa muhtasari na ukweli fulani (Mchepange, 2019). Mchepange anafafanua zaidi kuwa misemo mingi huibuka na kutumika kulingana na muktadha fulani wa kijamii. Katika visasuli vya Wahaya

utafiti huu umebaini kuwa misemo katika visasuli vya Wahaya hutumika katika muktadha wa makuzi ya vijana. Msimuliaji anasema:

> **Kihaya:** *Embwa keshelebuka neigufa elemwa elyata.*
>
> **Kiswahili:** Mbwa akicheza na mfupa mwisho wake huupasua.

Dondoo hili linaonesha msemo unaotumiwa wakati wa ujenzi wa maadili na makuzi ya vijana wenye jinsia mbili tofauti yaani jinsia ya kike na jinsia ya kiume. Utafiti huu umebaini kuwa msemo wa mbwa akicheza na mfupa unawalenga zaidi vijana wadogo wa kike na kiume waliokulia mtaa mmoja au nyumba moja. Vijana wa aina hiyo wanaweza wakazoeana na wakawa karibu kwa kucheza pamoja, lakini wazazi na walezi wanaonywa kuwaangalia vijana wa aina hiyo maana wakikua kuelekea kwenye ubinti na uvulana wanaweza wakajenga hisia za kimapenzi. Oyaro (2019) anafafanua kuwa misemo hutumika kufanikisha dhamira zenye sifa ya kiutamaduni kulingana na jamii husika. Hivyo, kiutamaduni katika jamii ya Wahaya misemo katika visasuli inalenga zaidi kuendeleza dhamira ya ujenzi wa maadili na makuzi wa vijana wa kike na wa kiume.

**Matumizi ya Taswira**

Uchambuzi wa data katika makala hii umebaini kuwa taswira ni kipengele kimojawapo cha sanaa kinachotumiwa katika visasuli vya Wahaya kujenga dhamira. Kulingana na Mulokozi (1996), Ntarangwi (2004), na Senkoro (2011) taswira ni ile hali ya mtunzi kueleza jambo au kitu fulani kwa wasomaji na wasikilizaji wake kwa kuchora picha ya kitu, hali, wazo, dhana au uzoefu katika akili zao. Aidha, utafiti huu umeonesha msimuliaji anaposimulia anamjengea taswira msikilizaji ajione kuwa kashuhudia kuona umbo la jitu, mahali au msichana mrembo. Hili linadhihirisha taswira ya mfupa kama ilivyo katika data ifuatayo:

> *Eigufa* – mfupa

Katika dondoo hili utafiti huu umebaini kuwa msimuliaji wa kisasuli katika kabila la Wahaya hutumia taswira ya mfupa kumaanisha mtu mwenye roho ya huruma kwa watu wenye shida. Aidha, taswira hutegemea upekee wa jamii husika kwa sababu jamii hutofautiana kiutamaduni, kimazingira na kimaingiliano na jamii nyingine (Badru, 2019). Aidha, msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa matumizi ya taswira hiyo huzingatia jinsia, umri na mahusiano yenye lengo la kuhakikisha usalama kwa watu na kwa jamii kwa ujumla.

**Dhamira Zinazojengwa na Vipengele vya Sanaa Kutoka Visasuli vya Wahaya**

Katika sehemu hii, utafiti huu umewasilisha dhamira zinazojengwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vya Wahaya. Dhamira zilizochambuliwa na kubainishwa zimewasilishwa katika sehemu inayofuata kama ifuatavyo:

**Dhamira ya Ukweli na Uwazi**

Utafiti huu umebaini kuwa kupitia kipengele cha kisanaa cha tafsida, dhamira ya ukweli na uwazi imejengwa. Abdalla (2018) anaeleza kuwa ukweli na uwazi ni ile hali ya mtu kusema neno kama lilivyo bila ya kuficha kitu au kuona aibu yoyote. Suala hili limethibitishwa na msimuliaji wa kisasuli cha Wahaya "nikwo nkola agwao tinkolelwa'ntyo" maana yake ndivyo ninavyofanya hukutana na sifanyiwi hivyo, aliposema:

> **Kihaya:** *Abakozi bamugambila Omukama bati otalila waitu naichwe nikwo tushasha katubona abalumuna baitu mbafa batyo, oyegumisilize.*
>
> **Kiswahili:** Wafanyakazi walimwambia Mfalme kuwa usilie na sisi ndivyo tunavyoumia tukiona ndugu zetu wanakufa hivyo, jikaze.

Dondoo hili inatuonesha katika kisasuli cha Kihaya kujenga dhamira inayoonesha umuhimu wa ukweli na uwazi kuwa kitendo chochote kibaya utakachomfanyia mwenzio iko siku kitakurudia mwenyewe. Hapa anajengwa mwanajamii kutofanya ubaya kwa mtu. Naye Benjamini (2019) anafafanua zaidi kuwa sanaa hutufunulia hali zetu za sasa za kijami, na pia hututayarisha kwa mabadiliko ya kijamii. Msingi wa Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji unaodai kuwa maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji huathiri usomaji na ufasiri wa kazi ya fasihi, umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa suala la kifo ni suala lisililozoeleka.

**Kuharibika kwa Maadili**
Kupitia uchambuzi wa visasuli teule vya Wahaya, imebainika kuwa kipengele cha sanaa cha kisitiari kinatumika katika jamii ya Wahaya kwa lengo la kuonesha mmomonyoko wa maadili. Dhana ya maadili imeelezwa na Chuachua (2016) kuwa ni seti ya mambo yanayotakiwa kufanywa na mwanajamii. Makala hii imebaini kuwa mbinu ya sanaa ya sitiari katika visasuli vya Kihaya imetumika kuonesha namna mmomonyoko wa maadili ulivyowaathiri watoto. Mtoa taarifa anasema:

> **Kihaya:** *Abana ba bilebi ni kabuzi wesibule.*
>
> **Kiswahili:** Watoto wa siku hizi ni mbuzi aliyekata Kamba.

Katika data hii imebainika kuwa suala la mmomonyoko wa maadili ni suala lililokatiwa tamaa na wazazi kwani halioneshi matumaini ya kurejea kama awali. Katika kisasuli cha Wahaya, mbinu ya sanaa ya kisitiari imemlinganisha mtoto na kamba ya mbuzi iliyokatika kwa maana ya uharibifu mkubwa wa maadili kwa watoto. Mwanazuoni Kabiru (2013) anadai kuwa kitendo cha wanajamii kukumbatia tamaduni za kigeni zilizokuja na utandawazi kumepoteza thamani ya maadili iliyofungamanishwa katika mila na desturi za jamii husika. Hivyo, muingiliano wa tamaduni ni chanzo kikubwa cha mmomonyoko wa maadili katika jamii.

**Suala la Utamaduni**
Kipengele cha tafsida kimetumika kujenga dhamira ya utamaduni katika kisasuli cha Wahaya. Utamaduni ni mfumo au utaratibu wa maisha ambao jamii inaufuata katika maisha yake ya kila siku ikijumuisha mila na desturi (Ramadhani, 2013). Aidha, utafiti huu umebaini kuwa suala la utamaduni katika visasuli vya Wahaya ni muhimu katika kuendeleza amali ya maadili ya jamii husika kwa kurithisha kizazi hadi kizazi. Suala la utamaduni limedhihirishwa na mtoa taarifa alipotumia tafsida ifuatayo:

> **Kihaya:** *Olwo yabaile nanjuna emyenda yona ekaba ejobile olwekyo naikala busha.*
>
> **Kiswahili:** Alipokuwa ananisaidia nguo zote zilikuwa zimeloa kwahiyo nilikuwa uchi.

Dondoo hili linaonesha wazi kuwa tafsida katika visasuli vya Wahaya ni miiko ya msingi hususani unapotamka viungo vya mwili kutegemeana na jinsia. Aidha, Sikuomba na Godfrey (2023) wanaeleza kuwa tafsida zina dhima za msingi katika kuendeleza mila, utamaduni na desturi za mawasiliano katika jamii. Kuheshimu utamaduni kulimfanya binti kukosa kuolewa ili kutunza heshima ya mama. Kupitia maarifa ya kimsingi na tajriba aliyonayo msomaji wa kazi ya fasihi, mtafiti amebaini kuwa katika jamii ya Wahaya ni mwiko mkwe kuona uchi wa mama mkwe wake. Hali hii ilimfanya binti wazuiliwe kuolewa kulingana na miiko ya jamii ya Wahaya.

**Dhamira ya Uzazi**
Uchambuzi wa data katika Makala hii umebaini kuwa mbinu ya methali katika visasuli vya Kihaya hutumika kujenga dhamira ya uzazi. Methali ni semi za kimapokeo zinazokumbukika na zenye muundo fulani unaotambulika na wanajamii na unaoelezea uzoefu unaokubalika na wanajamii kama ukweli fulani (Wamitila, 2008) anaeleza kuwa suala la uzazi katika jamii za Wabantu ni la msingi kwani ni ishara ya utajiri na kuacha kumbukumbu kwa jamii endapo wazazi watafariki. Hili linathibitika kupitia mtoataarifa aliposema:

> **Kihaya:** *Obushasi bwomwana bumanywa nyina.*
>
> **Kiswahili:** Uchungu wa mtoto aujuaye ni mama.

Dondoo hii inaonesha kuwa suala la uzazi ni suala la kuthaminiwa. Uthamani wake huwa tofauti kati ya mzazi ambaye tayari ana mtoto na yule ambaye bado hajapata mtoto, au kapata mtoto kamtupa. Faustini (2019) anaeleza kuwa Waafrika hutazama uzazi kama kigezo muhimu kinachoashiria uimara wa ndoa. Tofauti na utafiti huu ni kwamba, suala la uchungu wakati wa kujifungua ndiyo linapewa uzito kuliko uzazi kwa ujumla wake. Kwa hiyo, kupitia msemo huu ni wazi kuwa katika jamii ya Wahaya suala la uchungu aupatao mwanamke wakati wa kujifungua ndiyo unaopaswa kuheshimiwa zaidi hususani na watu ambao bado hawajazaa kwani hawawezi kuhisi uchungu huo.

**HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**
**Hitimisho**: Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira zinazojengwa na vipengele vya sanaa katika visasuli vya Wahaya. Dhamira zilizochunguzwa zinatokana na mbinu za kisanaa zinazotumiwa katika visasuli vya Wahaya. Katika uchambuzi wa vipengele vya sanaa katika visasuli

vya Wahaya, tumeona kwamba kuna vipengele vya sanaa kama vile: tashibiha, takriri, sitiari, tafsida, methali, kejeli, misemo na methali. Matokeo ya data zilizokusanywa yameonesha kuwa vipengele hivyo vya kisanaa vinaibua dhamira kama vile, ukweli na uwazi, kuharibika kwa maadili, suala la utamaduni pamoja na dhamira ya uzazi. Vilevile, Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ndiyo iliyotumika wakati wa kuchambua vipengele vya kisanaa katika visasuli vya Wahaya pamoja na dhamira zinazojengwa na vipengele hivyo. Kwa mantiki hiyo, ni wazi kuwa vipengele vya kisanaa vimetumika kujenga dhamira zenye kuakisi kwa karibu utamaduni wa jamii ya Wahaya. Si hivyo tu, bali utamaduni unaoakisiwa umelenga zaidi kuadilisha na kukuza maadili faafu toka kizazi kimoja hadi kingine. Aidha, kutokana na matokeo yaliyoelezwa katika Makala haya, kuna haja pia ya kuchunguza zaidi kuhusiana na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanavyotumika kukuza visasuli vya jamii ya Wahaya. Kwani licha ya sayansi kuwa na matokeo hasi bado jamii haiwezi kukwepa mchango wake katika kukua ana kuenea kwa visasuli vyake kama sehemu ya kutambulisha utamaduni wake.

**Mapendekezo:** Uchunguzi huu unapendekeza kuwa ili kuibua zaidi visasuli vya kabila la Wahaya, tafiti zaidi zijikite katika kuchunguza kipengele cha matumizi ya lugha hususani misemo na methali vinavyotumiwa katika visasuli kujenga na kuendeleza utamaduni wa jamii ya Wahaya hususani wakati huu wa maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Aidha, utafiti huu unapendekeza kufanyika kwa uchunguzi utakaojikita katika kuibua vipengele vya fasihi simulizi vinavyoendelezwa katika visasuli vya kabila la Wahaya. Hii itasaidia kuonesha uhai wa fasihi simulizi kupitia visasuli hususani katika kipindi hiki cha maendeleo ya sayansi na teknolojia.

Kadhalika, utafiti huu unapendekeza kuwa kupitia visasuli vya kabila la Wahaya tafiti ziende mbele zaidi katika kuchunguza uhusiano uliopo baina ya ubadilikaji wa mandhari na jamii unavyoweza kuibua visasuli vinavyokidhi matakwa ya hadhira lengwa hasa katika kipindi cha maendeleo ya sayansi na teknolojia.

## MAREJELEO


Abdalla, I. (2018). *Nafasi ya mwanamke katika fasihi simulizi*. Dar es Salaam: TUKI.

Badru, Z. A. (2019). Dhima ya taswira katika ufasiri na uteguzi wa vitendawili. *Kioo cha Lugha, 17,* 179–198.

Benjamini, A. (2019). *Mitazamo ya kijamii katika fasihi simulizi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Chuachua, B. (2016). *Ufundishaji wa fasihi kwa shule za sekondari*. Dar es Salaam: Open University of Tanzania.

Fadaee, E. (2006). Symbols, metaphor and simile in literature: A study of *Animal Farm*. *Journal of English and Literature, 2*(2), 19–27.

Faustine, S. (2019). Uafrikanishaji katika riwaya ya Kiswahili. *Mulika, 38,* 55–73.

Fish, S. (1980). *Is there a text in this class? The authority of interpretive communities*. Cambridge, MA: Harvard University Press.

Holub, R. C. (1984). *Reception theory: A critical introduction*. London & New York: Methuen.

Hussain, R. (2014). Metaphors and simile in literature. *International Journal of Humanities and Social Sciences Invention, 3*(9), 1–2.

Iser, W. (1978). *The act of reading: A theory of aesthetic response*. Baltimore, MD: Johns Hopkins University Press.

Jauss, H. R. (1982). *Toward an aesthetic of reception*. Minneapolis, MN: University of Minnesota Press.

John, B. N. (2023). Tafsiri ya lugha ya ishara katika *Wema Hawajazaliwa*: Mtazamo wa ulinganifu wa kimawasiliano. *Kioo cha Lugha, 21*(1), 143–159.

Kabiru, M. (2013). *Athari za mabadiliko ya kisiasa katika fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Kandagor, D. R. (2013). *The economic and social impact of land tenure systems in Kenya*. Eldoret: Moi University Press.

Khatib, R. M. (1999). *Fasihi ya Kiswahili: Nadharia na mifano*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Kitundu, G. J., & Malangwa, P. S. (2019). Ujenzi wa maana katika sitiari na tashibiha za Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, *17*, 75–98.

Maitaria, J. N. (2013). Methali katika ushairi wa Shaaban Robert. *Mulika*, 1–13.

Mbaabu, I. (2018). *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Mchepange, S. O. (2019). Misemo ya 'Vyuma Vimekaza': Uchambuzi wa mtindo na dhima yake. *Kiswahili*, *82*(1), 106–120.

Mgunda, J. M. (2004). Dhima ya visasili katika kuhifadhi na kurithisha amali za kitamaduni: Mifano kutoka kwa Wasukuma (Tasinifu ya MA Kiswahili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mrikaria, S. E. (2010). Kejeli na fasihi ya Kiswahili – Tanzania. *Swahili Forum*, *17*, 104–125.

Mulokozi, M. M. (2017). *Utangulizi wa fasihi ya Kiswahili: Kozi ya fasihi vyuoni na vyuo vikuu*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Mulokozi, M. M. (1996). *Theory and practice of oral literature*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Nguti, R. (2013). *Uchanganuzi wa matumizi ya lugha katika fasihi ya Kiswahili*. Nairobi: Focus Publications.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa kazi za fasihi*. Rock Island, IL: Augustana College.

Okpewho, I. (1992). *African oral literature: Background, character and continuity*. Bloomington, IN: Indiana University Press.

Omari, I. M. (2006). *Educational research: Concepts and methods*. Dar es Salaam: Delah Educational Publishers.

Oyaro, B. (2019). Maana na matumizi ya misemo katika lugha ya Kiswahili. *Jarida la Kiswahili*, *15*(2), 45–67.

Ramadhani, S. K. (2013). Usawiri wa wanawake katika taarabu ya mipasho: Mfano kutoka nyimbo za Mzee Yusufu Mzee (Tasinifu ya MA Kiswahili, haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU.